KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

# MIFUMO YETU

Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI

TOLEO NA. 2 • AGOSTI-OKTOBA 2017



# Mfumo Mpya wa Uhasibu na Utoaji wa Taarifa za Fedha katika Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS)



*Picha ya mbele: Watumishi wanaohusika na kutoa taarifa za mahesabu katika shule yao iliyopo kwenye Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wakifuatilia mafunzo ya Mfumo wa Uhasibu na Utoaji Taarifa za fedha kwa Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS), kutoka kwa Mratibu wa Elimu jijini humo. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision).*

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*" Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya Ofisi ya Rais—TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani"*

USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

UHURU NA UMOJA

# Bodi ya Uhariri

## Mwenyekiti

*Eng. Mussa Iyombe*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Baltazari Kibola – TAMISEMI*
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Matiko Machonchoryo – PS3*
*Gemini Mtei – PS3*

## Waandishi

*Mathew Kwembe – TAMISEMI*
*Atley Kuni – TAMISEMI*
*Gladys Mkuchu – PS3*
*Jacqueline Sombe – PS3*

## Mhariri Mkuu

*Leah Mwainyekule – PS3*

## Wahariri

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Mathew Kwembe – TAMISEMI*

## Msanifu Kurasa

*Nteghenjwa Hosseah – TAMISEMI*



## Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*

## Ndani ya Jarida Hili:

**Tahariri……………………………………………………………………….uk 6**

**Waratibu Elimu Kata, Waganga Wapewa Elimu ya Uhasibu………………uk 7**

**FFARS Yarahisisha Upatikanaji Taarifa Sahihi……………………………..uk 8**

**Mfumo wa Uhasibu Kuchochea Uwazi na Uwajibikaji………………………uk 9**

**Tanzania Yaipongeza Marekani ……………………………………………uk 10**

**PS3 Yaboresha Mfumo wa Uhasibu na Utoaji wa Taarifa ………………….uk 11**

**Wahasibu wa Elimu, Afya Waaswa……………………………………………..uk 12**

**Mfumo Mpya wa Uhasibu kupungua Hati zenye Mashaka…………………uk 13**

**Miradi Inayofadhiliwa Hapa Nchini Ifanyiwe Tathmini……………………..uk 14**

**Watakiwa Kuthamini Mchango wa USAID………………………………...uk 15**

**FFARS Yaleta Suluhu ya Hesabu za Fedha…………………………………...uk 16**

**FFARS Kuchochea Huduma Bora za Afya, Elimu……………………………uk 17**

**PS3 Yazidi Kung’ara Katika Halmashauri Tanzania ………………………..uk 18**

*TAHARIRI:*

# Mwarobaini wa Upotevu wa Fedha za Umma Wapatikana

Moja ya malengo mahususi ya kuanzishwa kwa Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma hapa nchini, ni kuona namna ya kuinua ufanisi katika mapato na matumizi ya rasilimali za fedha Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo kuu la Mradi huu ujulikanao kwa lugha ya Kiingereza kama Public Sector Systems Strengthening (PS3), ni kuwezesha wananchi kupata huduma stahiki kwenye maeneo yao.

Hata hivyo, ili hayo yote yafanikiwe, ni lazima nchi iwe na Serikali makini yenye uwezo wa kukusanya kodi na kutumia mapato hayo kwa uadilifu, na kwa malengo yaliyokusudiwa.

Jambo la kukumbukwa hapa ni kwamba Serikali hupata rasilimali fedha kwa kuwatoza raia wake kodi, ushuru na ada mbalimbali ambazo baadaye hutumika katika kuwaletea wananchi maendeleo. Maendeleo haya ni pamoja na uboreshaji wa huduma za elimu, maji, miundombinu bora, umeme wa uhakika na zaidi kuboresha ustawi wa wananchi ambao kimsingi ndiyo wanaobeba dhamana ya Serikali iliyopo madarakani.

Kuwepo kwa uadilifu wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali kwa nchi yoyote ile duniani kunaenda sanjari na kuwa na watumishi na viongozi wenye maadili na nidhamu ya fedha ambao hawatangulizi ubinafsi katika kutunisha matumbo yao kwa kupora fedha za walipa kodi.

Ni kwa mantiki hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Mradi wa PS3 imeanzisha mfumo mpya wa uhasibu na utoaji wa taarifa kwenye vituo vya kutolea huduma, unaojulikana kwa lugha ya Kiingereza kama *Facility Financial Accounting and Reporting System* (FFARS).

Mfumo huo utasaidia utekelezaji wa utoaji wa raslimali fedha moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma hapa nchini, kwa kuwapatia watoa huduma mfumo sanifu uliorahisishwa ambao utawawezesha kutunza taarifa za fedha zinazotolewa na zilizopo kwenye vituo vya kutolea huduma.

Jambo la faraja ni kwamba FFARS sasa itaiwezesha nchi kuwa na ufanisi wa utendaji katika utoaji wa huduma kwa ufanisi, ambapo utekelezaji wake umeanza kwenye vituo vya kutolea huduma, hususani kwenye sekta za elimu na afya hapa nchini.

Ni hatua muhimu sana kwa upande wa Serikali kuhakikisha kwamba mfumo huo utakuwa na faida nyingi kwa taifa, kwa sababu utakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa vituo vyote vya kutolea huduma vinakusanya na kuhifadhi taarifa za mapato na matumizi zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya vituo hivyo, ili wananchi waweze kunufaika na raslimali fedha kwa kupatiwa huduma bora. Hali hii itachangia uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi na matumizi sahihi ya fedha za umma.

Kwa upande wa elimu, kwa mfano, matumizi ya mfumo wa FFARS yatasaidia kuhakikisha kwamba fedha kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa shule kama vile kununua vifaa vya kufundishia zinatumika ipasavyo, na hivyo kuwawezesha wanafunzi kupata elimu bora. Halikadhalika, kwa upande wa sekta ya afya, FFARS itasaidia kuhakikisha kwamba ruzuku itakayotolewa itasaidia kuwezesha upatikanaji wa vifaa tiba ambao utaainishwa katika taarifa za matumizi ya kituo husika na hivyo kusaidia wananchi kupata huduma bora za afya.

Jarida hili limetanabahisha namna mafunzo ya FFARS yalivyoendeshwa nchini kote pamoja na faida zake, na jinsi mfumo huo – ukitumika ipasavyo – unavyoweza kuwa mwarobaini wa kuzuia upotevu wa fedha za umma.

Tunawatakia usomaji mwema!

**Eng. Mussa Iyombe**
**Katibu Mkuu, OR-TAMISEMI**

## KUTOKA MTWARA:

# Waratibu Elimu Kata, Waganga wa Vituo vya Afya Wapewa Elimu ya Uhasibu

Waganga wafawidhi wa vituo vya afya, na waratibu elimu kata kutoka Halmashauri 93 zilizo katika mikoa 13 nchini inayotekeleza Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), wamepata mafunzo ya namna ya kutumia mfumo mpya wa uhasibu na utoaji taarifa za fedha katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma, unaojulikana kwa Kiingereza kama *Facility Financial Accounting and Reporting System* (FFARS).

Kwa mujibu wa Mkuu wa Timu ya Mifumo ya TEHAMA wa PS3, Bw. Desderi Wengaa, mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma na kusaidia upatikanaji wa taarifa sahihi katika mahesabu ya mapato na matumizi ya Halmashauri. Mafunzo ya FFARS yamefadhiliwa na Watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la marekani (USAID).



***Baadhi ya watumishi wa Shule ya Sekondari ya Loleza jijini Mbeya, wakipata mafunzo ya FFARS kutoka kwa Mratibu wa Elimu Kata jijini humo. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision)***

Bw. Wengaa amesema kwamba kuundwa kwa mfumo huo kutasaidia kuhakikisha fedha za ruzuku zinasimamiwa vizuri na taarifa za matumizi yake zinatolewa kwa usahihi, tofauti na ilivyokuwa mwanzo.

Amesema kuwa FFARS itawapatia watoa huduma mfumo sanifu uliorahisishwa ambao utawawezesha kutunza taarifa za fedha zinazotolewa na zilizopo katika vituo vyao, na kuongeza kwamba FFARS itaweza kufuatilia matumizi ya fedha hizo katika kufikia malengo ya utoaji huduma na kuhakikisha yanaendana na sheria za manunuzi na utoaji taarifa.

“Taarifa hizi zitasaidia Serikali kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha za umma na kuongeza uwazi, na hivyo watoa huduma wa afya kuwa na wajibu kwa jamii wanayoihudumia,” ameeleza.

Wengaa alitanabahisha kwamba mafunzo hayo yanafanyika katika mikoa 13 ya Tanzania bara inayotekeleza Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), ambapo waratibu elimu kata na waganga wafawidhi wa vituo vya afya wanashiriki. Mikoa hiyo 13 ni Mtwara, Lindi, Dodoma, Iringa, Mbeya, Njombe na Morogoro, Mara, Mwanza, Rukwa, Shinyanga, Kigoma, na Kagera.

Mafunzo hayo yanafanyika katika ngazi ya Halmashauri, ambapo mjini Mtwara mafunzo hayo yaliwahusisha waganga wafawidhi wa vituo vya afya, na Waratibu elimu kata kutoka Halmashauri za Manispaa ya Mtwara Mikindani na Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara.

Akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani, Bibi Beatrice Dominick, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Mhandisi Sambwe Sijabaje amesema kwamba mafunzo hayo yatawasaidia watoa huduma wa vituo vya Halmashauri hizo mbili kuwa na mfumo maalum wa kuandaa taarifa za mapato na matumizi, na hivyo kuchangia uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mafunzo hayo, amesema, yanatolewa kwa mfumo wa kielektroniki ili kuendana na wakati na mabadiliko ya teknolojia. Vilevile, mafunzo pia yanatolewa kwa kutumia mfumo wa kujaza vitabu ulioboreshwa ili kukidhi changamoto mbalimbali za miundombinu ikiwemo umeme na kukosekana kwa huduma ya mtandao wa intaneti kwa baadhi ya vituo vya kutolea huduma.

Mfumo huo wa FFARS unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI); Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, pamoja na USAID/PS3.

Mafunzo hayo yanatarajiwa kuwanufaisha waganga wafawidhi wa vituo vya afya, na waratibu elimu kata kutoka zaidi ya Vituo vya Afya 550, Zahanati 6800, Hospitali za Wilaya 135, na takribani Shule za Msingi na Sekondari 20,000 katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

***Imeandikwa na Mathew Kwembe, OR-TAMISEMI***

*KUTOKA DODOMA:*

# FFARS Yarahisisha Upatikanaji Taarifa Sahihi za Fedha Vituoni

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeeleza kuwa mfumo wa kupeleka fedha moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma umeiondolea ugumu wa kupata taarifa sahihi za matumizi halisi ya fedha zinazopelekwa kwenye vituo hivyo.

Akizungumza katika mahojiano maalum na jarida hili, Afisa Msimamizi wa Fedha Mwandamizi kutoka OR- TAMISEMI, Bw. Elisa Rwamiago, amesema kuwa mfumo huo utakuwa na msaada mkubwa kwa ofisi yake kwani utaisaidia Serikali kufanya tathmini ya matumizi ya fedha na kusaidia katika kupanga mipango na bajeti za fedha kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma.

Amesema kuwa mfumo wa FFARS utaisaidia Serikali kuwa na takwimu sahihi ya kuweza kujua namna mapato yanavyotumika katika ngazi za msingi, lakini pia kujua mapato yanayopotea na kuweza kudhibiti kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

"Mfumo huu umetengenezwa kudhibiti matumizi ya fedha kinyume na mipango iliyokusudiwa, kwa sababu inavitaka vituo kutoa taarifa za uhasibu za matumizi kulingana na namna kila fungu lilivyotengwa kwa kazi maalum tu na bila kuhamisha matumizi," ameeleza.

Bwana Rwamiago ameongeza kuwa kuundwa kwa mfumo wa FFARS ni hatua ya maendeleo katika kufanikisha usimamizi wa fedha za umma ambao upo katika mfumo uliorahisishwa.

"Tofauti na awali, sasa kutakuwa na mfumo uliorahisishwa wa kujaza kwenye madaftari ya fedha, lakini pia na mfumo wa kielektroniki ambao utasaidia sana kutoa taarifa na miongozo hata kwa wakaguzi ili kurahisisha kazi zao katika kukagua matumizi ya fedha katika vituo hivi vya kutolea huduma," amesisitiza Bwana Rwamiago.

> ***"Mfumo huu umetengenezwa ili kudhibiti fedha kutumika kinyume na mipango iliyokusudiwa"*** **- Elisa Rwamiago, OR-TAMISEMI**

Ameongeza kuwa mfumo huo pia utachangia kuboresha uwazi kwa sababu wananchi watapata taarifa sahihi juu ya matumizi ya vituo vyao, lakini pia kuwezesha watendaji na viongozi kama vile Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa na Viongozi wa Wizara husika kuona nini kinaendelea katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma.

"Mfumo huu utawezesha mtu yoyote mwenye uwezo wa kuingia na kujua taarifa hizo, lakini pia itachangia uwajibikaji kwa wananchi ambao ndio wanaohitaji huduma hizi," ameeleza.

"TAMISEMI inawashukuru PS3 kuwa na mradi wenye matokeo. Kwa miaka miwili sasa tumekuwa tunashirikiana katika kuboresha mifumo mbalimbali ya sekta za Umma ili wananchi waweze kupata huduma bora," amesema.

***Imeandikwa na Gladys Mkuchu, PS3***



*Afisa Msimamizi wa Fedha Mwandamiizi kutoka Ofisi ya Rais—TAMISEMI, Elisa Rwamiago (kushoto) akifanyiwa mahojiano maalum na mwandishi wa habari hii. (Picha: Octavian Kimario, Idara ya Habari Maelezo)*

## *KUTOKA KIGOMA:*

# Mfumo wa Uhasibu na Utoaji Taarifa za Fedha Kuchochea Uwazi na Uwajibikaji

Serikali imesema kuwa kuundwa kwa mfumo mpya wa uhasibu na utoaji wa taarifa sahihi juu ya matumizi ya fedha za umma kutachochea uwazi na uwajibikaji, na kufanikisha lengo lililokusudiwa la kupeleka huduma bora kwa wananchi.




***Nakala ya mwongozo wa mafunzo ya Mfumo wa Uhasibu na Utoaji Taarifa katika Vituo vya Kutolea Huduma. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision)***

Akizungumza wakati wa mafunzo ya awamu ya pili ya Mfumo wa Uhasibu na Utoaji Taarifa za Fedha kwa ngazi ya kituo cha kutolea huduma, Mkurugenzi wa Wilaya ya Uvinza, Mhandisi Weja Lutobola Ng'olo, amesema mpango wa Serikali wa kupeleka fedha moja kwa moja kwa ngazi ya vituo vya kutolea huduma una lengo la kuhakikisha uwepo wa huduma bora kwa umma na kurahisisha upangaji wa mipango na utoaji wa taarifa za matumizi ya fedha hizo.

Mhandisi Ng'olo ameongeza kuwa kufanya hivyo kutaimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha za umma na watoa huduma kuwa na wajibu kwa jamii wanayoihudumia kwa kutoa huduma bora.

"Hivyo nawaasa mtakapoenda kutoa mafunzo haya kwa watoa huduma muwasisitize juu ya umuhimu wa kuwa wazi katika kutoa taarifa na kufahamu ya kuwa wana wajibu kwa wananchi wanaowahudumia," amesema.

Kwa upande wake, Dk Ernest Nsumila kutoka kata ya Kalya wilayani Uvinza ambaye alikuwa mshiriki wa mafunzo hayo amesema changamoto nyingi katika utoaji wa taarifa za fedha na matumizi katika vituo vya afya inatokana na Halmashauri kuwa waratibu wa mipango na matumizi ya fedha katika vituo.

Amesema kumekuwa na changamoto kutoka kwa wananchi kukosa huduma kama za vifaa tiba na dawa, lakini kupitia mfumo huu utaratibu utabadilika sana na vituo kuweza kupanga mipango yao wenyewe kulingana na mahitaji ya wananchi na hivyo kuboresha huduma zinazotolewa katika vituo hivyo.

Naye Mratibu wa Elimu Kata ya Uvinza, Bi Rachel Shilly, amesema mpango wa Serikali wa kuleta fedha katika sekta ya elimu umeshaanza kupitia mpango wa elimu bila malipo, lakini kumekuwa na changamoto nyingi sana kutokana na walimu wanaoshughulikia utoaji wa taarifa na matumizi kukosa uelewa mpana zaidi juu ya utoaji taarifa za fedha na namna ya kuratibu matumizi. Kutokana na hilo, amesema, pesa hazikutumika kwa ajili ya lengo lililowekwa na hivyo kuathiri utoaji huduma katika shule.

***Imeandikwa na Gladys Mkuchu, PS3***

*KUTOKA MARA:*

# Tanzania Yaipongeza Marekani Kuwajengea Uwezo Watoa Huduma

Serikali wilayani Serengeti imeipongeza Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Kimataifa la Maendeleo (USAID) kwa kutoa mafunzo ya mfumo wa uhasibu na taarifa za fedha kwa ngazi ya vituo vya kutolea huduma.

Pongezi hizo zimetolewa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, Simion Waryoba, wakati alipokuwa akifungua mafunzo hayo.

Ameushukuru pia uongozi wa Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma, ujulikanao kwa Kiingereza kama *Public Sector Systems Strengthening* (PS3) kwa kuwezesha na kuleta mafunzo hayo kwa wakuu wa vituo hivyo kwa ufadhili wa watu wa Marekani kupitia USAID.

"Tunaishukuru sana Serikali ya Marekani na watu wake kwa kufadhili mafunzo haya ambayo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu," amesema.

Mafunzo hayo yanatolewa kwa wakuu hao wa vituo ili kuwawezesha kwenda kuwafundisha watoa huduma mbalimbali walioko kwenye vituo vyote vya kutolea huduma Tanzania Bara, vinavyojumuisha zahanati, vituo vya afya, hospitali, shule za sekondari na msingi.

"Mafunzo haya yatachangia uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi, kwa kuangalia matumizi bora ya fedha," amesema.

Hata hivyo, Waryoba amekiri kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa taarifa sahihi za rasilimali fedha kwenye vituo vya kutolea huduma na hivyo kushindwa kutoa taarifa sahihi za matumizi ya fedha za ruzuku zinazotolewa katika vituo hivyo.

"Hali hii wakati mwingine husababisha Halmashauri kupata hati ya mashaka kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali," amebainisha.


Amesema mfumo huo mpya wa utoaji wa taarifa za fedha utasaidia kuwepo kwa muundo maalum wa kuhifadhi taarifa za mapato na matumizi kwa kuongeza uwazi na uwajibikaji wa wakuu wa vituo vya kutolea huduma na hivyo kupunguza changamoto zilizokuwepo siku za nyuma.

> ***"Hali hii wakati mwingine husababisha Halmashauri kupata hati ya mashaka kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali"*** **- Simion Waryoba, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti**

"Ni imani yangu kwamba baada ya mafunzo haya, vituo hivi vitatoa taarifa sahihi, ambazo zitasaidia mwananchi kuhoji pale atakapoona kuwa huduma zinazotarajiwa kutolewa kwenye vituo hazitolewi kulingana na ruzuku iliyotolewa," amefafanua.

Kwa upande wake, Mratibu wa PS3 Wilaya ya Serengeti, Martin Mlelema, amesema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watoa huduma kwenye vituo vya kutolea huduma na kusaidia upatikanaji wa taarifa sahihi za hesabu kwenye Halmashauri.

***Na Nashon Kennedy wa Habari Leo***




***Mratibu wa Elimu Kata kutoka Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma akitoa mafunzo kwa watumishi wanaojihusisha na masuala ya fedha katika Shule ya Msingi Buhigwe. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision)***

*KUTOKA DAR ES SALAAM:*

# PS3 Kuboresha Mfumo wa Uhasibu na Utoaji Taarifa katika Vituo vya Kutolea Huduma



***Mwananchi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma akiuruahia habari kwamba Serikali itaanza kutuma hela moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision)***

Mapungufu katika mfumo wa usimamizi wa fedha za umma na utoaji taarifa katika ngazi ya mtoa huduma, imepelekea Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kupitia mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi; na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuja na mfumo mpya.

Mfumo huo mpya ni wa uhasibu na utoaji taarifa, unaojulikana kwa Kiingereza kama *Facility Financial Accounting and Reporting System* (FFARS).

Mkuu wa Kitengo cha Mifumo ya Fedha PS3, Dkt. Gemini Mtei, amesema kupitia mpango wa Serikali wa kupeleka fedha moja kwa moja katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma inayojumuisha zahanati, vituo vya afya, hospitali pamoja na shule za msingi na sekondari, ilionekana ni vyema kuja na mfumo mpya wa uhasibu na utoaji taarifa ambao utasaidia usimamizi wa fedha na kuhakikisha kuwa zinatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa.

"Mfumo huu wa uhasibu na utoaji taarifa umerahisishwa zaidi na uko katika aina mbili, yaani mfumo wa kielektroniki na mfumo wa zamani ulioboreshwa wa kujaza katika vitabu kwa vituo ambavyo havina mawasiliano ya mtandao. Hii itawezesha kila kituo Tanzania nzima kuweza kutekeleza mpango huu, na utarahisisha na kuongeza ufanisi katika mifumo ya Serikali ya Tanzania na kuboresha usimamizi na matumizi ya rasilimali za umma," ameeleza Dkt. Mtei.

Amesema mfumo huu utawezesha utoaji taarifa za kila mwezi, tofauti na awali ambapo taarifa zilikuwa zinatolewa kila baada ya robo mwaka. Mfumo huu mpya utachochea uwazi kwa vituo hivi vya kutolea huduma, lakini pia utaongeza uwajibikaji kwa wananchi wanaowahudumia na hivyo kuchochea upatikanaji wa huduma bora na stahiki.

Lengo la mfumo huu ni kuwezesha vituo vya kutolea huduma kutoa huduma bora kulingana na mahitaji ya wananchi wanaowahudumia. Kutokana na hilo, Dkt. Mtei amesema mfumo huu wa FFARS utawezesha kubainisha matumizi ya rasilimali zilizopo na kuweka vipaumbele vya mahitaji ya huduma kulingana na uhitaji wa huduma hizo, tofauti na awali ambapo mipango ya fedha ilikuwa inatoka Halmashauri na hivyo kuvifanya vituo kutokuwa na maamuzi ya mipango na matumizi kulingana na mahitaji ya wananchi.

Dkt. Mtei ameongeza kuwa kufuatia mafunzo ya awali yaliyotolewa na PS3 kwa watoa huduma, ni imani ya kila mmoja kwamba mpango huu wa Serikali utatekelezwa na kuwa endelevu, na mfumo huu utaiwezesha Serikali kuwa na taarifa sahihi juu ya matumizi ya rasilimali fedha zinazotolewa katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma. "Hili litawezesha upangaji wa bajeti ya Serikali na kuweka vipaumbele kulingana na mahitaji ya vituo na wananchi wanaowahudumia," amesisitiza.

***Imeandikwa na Gladys Mkuchu, PS3***

*KUTOKA SHINYANGA:*

# Wahasibu wa Elimu, Afya Waaswa Kufanya Kazi kwa Uadilifu

Mafunzo ya mifumo mbalimbali ya fedha yanayotolewa na wafadhili hapa nchini yataleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi endapo watalaam wa fedha watafanya kazi kwa uaminifu kwa kutoa taarifa sahihi za matumizi ya ruzuku zinazotolewa kwenye vituo vya kutolea huduma.

Hayo yamesemwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, wakati akifungua mafunzo ya siku mbili ya mfumo mpya wa uhasibu na utoaji taarifa za fedha kwenye vituo vya kutolea huduma (FFARS) kwa wahasibu wa idara ya elimu na afya kutoka mikoa ya kanda ya ziwa.

Amesema baadhi ya Halmashauri nchini zilikuwa na changamoto nyingi za kiutendaji kwenye mifumo ya utoaji taarifa na fedha, hali ambayo ilifanya sekta mbalimbali nchini, zikiwemo za elimu na afya kupata malalamiko mengi.

"Tulikuwa na shida ya upatikanaji wa takwimu kwa kisingizio cha kutokuwa na mfumo, lakini pia mtandao kwa baadhi ya maeneo hapa nchini. Ni matumaini yetu mtayatumia mafunzo haya kuleta mapinduzi ya kiuchumi," amesema.

Amebainisha kwamba lengo la mafunzo hayo yaliyowashirikisha wahasibu zaidi ya 400, ni kuwajengea uwezo watoa huduma kwenye vituo vya kutolea huduma, hususani katika sekta za afya na elimu, na hivyo kusababisha kupatikana kwa taarifa sahihi za fedha za mapato na matumizi za Halmashauri.

"Lengo ni kuhakikisha vituo vyetu vya kutolea huduma kupitia fedha za ruzuku vinakuwa na mfumo maalum wa kuandaa taarifa za mapato na matumizi, hali itakayochangia uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi, lakini pia fedha kutumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa," amefafanua.



***Mafunzo ya Mfumo wa Uhasibu na Utoaji Taarifa katika Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS) yakiendelea katika eneo la shule Wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision)***

Amesema awali kulikuwa na upotevu wa rasilimali fedha zilizokuwa zinatolewa kwenye vituo vya kutolea huduma, hali iliyosababisha Halmashauri kushindwa kutoa taarifa sahihi za matumizi ya ruzuku zilizokuwa zinatolewa kwenye vituo hivyo.

"Mfano ni sekta ya elimu ambapo tumeona kulikuwa na udanganyifu wa wanafunzi waliopo shuleni, waliopata ruzuku zaidi ya fedha na zingine kupotea mikononi mwa watu," ameeleza, na kuipongeza Serikali ya Marekani kwa kufadhili mafunzo hayo.

Kwa upande wake, Kaimu Mratibu wa Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) kwa Mkoa wa Shinyanga, Glory Mbia, amesema mfumo huo mpya wa kupatiwa raslimali fedha utatoa motisha kwa vituo vya kutolea huduma za afya na kuongeza kipaumbele cha utoaji huduma bora kwa wananchi kwa kuongeza usawa na uwazi.

"Upelekaji wa moja kwa moja wa fedha kwenye vituo vya kutolea huduma, utahakikisha fedha zinazotolewa na Serikali zinatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa," amesema.

Amesema PS3 inalenga kuimarisha mifumo ya sekta za umma na husaidia kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za umma na matumizi yake.


Mfumo wa FFARS unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Watoto na Walemavu na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID).

***Na Nashon Kennedy wa Habari Leo***

*KUTOKA MTWARA:*

# 'Mfumo Mpya wa Uhasibu Kupunguza Hati zenye Mashaka katika Halmashauri'

Serikali imesema kuanza kutumika kwa mfumo wa uhasibu na utoaji taarifa za fedha kwa ngazi ya kituo cha kutolea huduma kutapunguza changamoto za Halmashauri kupata hati zenye mashaka pindi zinapokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.




*Mchoro ukionyesha mfano wa kuutumia mfumo wa FFARS kwa njia ya kielektroniki, katika kituo cha kutolea huduma. (Mchoro: Nathan Mpangala)*

Mfumo huo utaiwezesha Serikali kupeleka rasilimali fedha moja kwa moja kwenye vituo vya afya kwa ngazi za Halmashauri. Vituo vya kutolea huduma ambavyo vitapokea fedha hizo vinajumuisha zahanati, vituo vya afya, na hospitali za wilaya. Zoezi hilo litaenda sambamba na inavyotekelezwa kwenye sekta ya elimu, Serikali za Vijiji na Ofisi za Kata.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara, Alfred Luanda, ameyasema hayo mjini Mtwara wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wakufunzi wa mfumo wa uhasibu na utoaji taarifa za fedha kwa ngazi ya kituo cha kutolea huduma kwa wahasibu kutoka Halmashauri za mikoa sita ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Tanga, Pwani na Dar es salaam.

Mafunzo kama hayo pia yamefanyika katika kanda nyingine za Mbeya, Dodoma, na Shinyanga, ambapo jumla ya wakufunzi 490 kutoka katika taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma ujulikanao kwa Kiingereza kama Public Sector Systems Strengthening (PS3), wanashiriki.

Luanda ameeleza kwamba kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa taarifa sahihi za rasilimali fedha zilizopo katika vituo vya huduma, na hivyo kusababisha Halmashauri nyingi nchini kushindwa kutoa taarifa sahihi za matumizi ya ruzuku zinazotolewa katika vituo hivyo.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia miundombinu, Elias Nyamusami, Katibu Tawala wa Mkoa ameongeza kuwa kukosekana kwa mfumo wa uhasibu na utoaji wa taarifa za fedha umezifanya Halmashauri zionekane kwamba zinasababisha kwa makusudi upotevu wa fedha.

"Ukweli ni kwamba hakukuwa na mfumo sahihi wa kuzisaidia Halmashauri kulizuia hilo," amesema.

Ameongeza kuwa mfumo huo mpya wa kupatiwa rasilimali fedha utatoa motisha kwa vituo vya kutolea huduma za afya na kuongeza kipaumbele cha utoaji huduma bora kwa wananchi wa Tanzania na kuongeza usawa na uwazi.

"Mfumo huu umetengenezwa kisasa, hivyo ni wa kielektroniki. Hata hivyo, mfumo wa kujaza katika vitabu na wenyewe umeboreshwa na kuwa rahisi kwa mtumiaji kujaza taarifa sahihi, na huu utatumika kwa vile vituo ambavyo changamoto ya upatikanaji wa miundombinu wezeshi katika matumizi ya kielektroniki," amesema na kuongeza kwamba mara baada ya kujaza katika vitabu, takwimu hizo zitaingizwa katika mfumo kwenye ngazi ya Halmashauri na vituo kupatiwa taarifa ya vituo vyao.

Alisema kuwa upelekaji wa rasilimali fedha moja kwa moja kwa vituo vya kutolea huduma utahakikisha kuwa fedha zinazotolewa na Serikali zinatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa. Mkakati huo mpya wa kuboresha sekta za afya na elimu ni msaada kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID).

Wakufunzi 490 wataweza kutoa elimu kwa watumiaji wa mwisho wa mfumo wa FFARS katika zaidi ya Vituo vya Afya 550, Zahanati 6,800, Hospitali za Wilaya 135, na takribani Shule za Msingi na Sekondari 20,000 katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, vikiwemo vituo vya kutolea huduma kutoka Mikoa 13 na Halmashauri 93 zinazotekeleza Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).

***Na Mathew Kwembe, OR-TAMISEMI***

## *KUTOKA SHINYANGA:*

# 'Miradi Inayofadhiliwa Hapa Nchini Ifanyiwe Tathmini '



***Mchoro ukionyesha mfano wa namna ya ujazaji wa mahesabu kwa njia ya kawaida ilyoboreshwa, katika eneo la shule. (Mchoro: Nathan Mpangala)***

WITO umetolewa kwa taasisi za Serikali na mashirika yanayotekeleza miradi mbalimbali inayofadhiliwa na wafadhili na washirika mbalimbali wa maendeleo hapa nchini kujenga mfumo wa kufanya tathmini ya miradi hiyo ili kuona kama inaleta tija.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Steven Magoiga, wakati alipokuwa akifungua mafunzo ya siku mbili ya Mfumo wa uhasibu na utoaji wa taarifa za fedha kwa ngazi ya vituo vya kutolea huduma (FFARS) kwa maafisa elimu kata na wakuu wa vituo vya afya wilayani hapo.

"Tufike mahala tuwe tunafanya tathimini ya miradi hii inayokuja kutekelezwa kwenye maeneo yetu ili tuone kama inaleta tija; tusipofanya hivyo si rahisi kufahamu kama lengo la mradi fulani limetimia na nchi imenufaikaje," amefafanua.

Amesema tathmini hiyo itakuwa ni dira kwa nchi katika kuelewa aina ya miradi iliyotekelezwa kwa ufanisi na kuwa kigezo kizuri cha kupata ruzuku ya fedha ya kuendeleza miradi mingine kutoka kwa wafadhili na washirika wa maendeleo.

Mafunzo hayo ya siku mbili yametolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma, *Public Sector Systems Strengthening (PS3)* kwa ufadhili wa Watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID).

Ameishukuru Serikali ya Marekani kwa ufadhili wa mafunzo hayo, ambayo yatawawezesha watumishi wa kada ya afya na elimu katika wilaya yake kufahamu namna ambavyo mifumo mbalimbali ya Serikali inavyofanya kazi, lakini pia kuwa na usimamizi madhubuti wa fedha na raslimali za umma.

"Kupitia mfumo huu, fedha za ruzuku zitasimamiwa vizuri kwa kuhakikisha kuwa taarifa za matumizi yake zinatolewa kwa usahihi tofauti na ilivyokuwa mwanzo," amesema.

Aidha ameongeza kuwa mafunzo hayo yatahakikisha kuwa vituo vya kutolea huduma kwa sekta za afya na elimu vinakuwa na mfumo maalum wa kuandaa taarifa za mapato na matumizi, hali itakayochangia uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Amekiri kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa taarifa sahihi za rasilimali fedha kwenye vituo vya kutolea huduma, na hivyo kufanya Halmashauri yake kushindwa kutoa taarifa sahihi za matumizi ya ruzuku zinazotolewa kwenye vituo hivyo.

"Kushindwa kutoa taarifa huku wakati mwingine kulisababisha Halmashauri kupata hati ya mashaka kutoka kwa Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali. Ukweli ni kwamba hatukuwa na mfumo sahihi wa kulizuia hilo," amesema.

Amesema kuwa mfumo huo mpya wa utoaji wa taarifa za fedha, utasaidia kuwepo kwa muundo maalum wa kuhifadhi taarifa za mapato na matumizi kwa kuongeza uwazi na uwajibikaji wa wakuu wa vituo vya kutolea huduma, na hivyo kupunguza changamoto zilizokuwepo siku za nyuma.

"Ni imani yangu kwamba baada ya mafunzo haya, vituo vitatoa taarifa sahihi ambazo zitasaidia mwananchi kuhoji pale atakapoona kuwa huduma zinazotarajiwa kutolewa kwenye vituo hazitolewi kulingana na ruzuku iliyotolewa," amefafanua.

Kwa upande wake, Meneja wa PS3 mkoa wa Kagera, Shishira Mnjokava, amesema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watoa huduma katika vituo vyote vya kutolea huduma na kusaidia upatikanaji wa taarifa sahihi kwenye mahesabu ya mapato na matumizi ya Halmashauri nchini.

***Na Nashon Kennedy wa Habari Leo***

## KUTOKA RUKWA:

# Waratibu Elimu Kata, Maafisa Afya Watakiwa Kuthamini Mchango wa USAID

Waratibu wa elimu kata na maafisa afya mkoani Rukwa wametakiwa kuthamini mchango wa USAID katika kuwaletea mafunzo ya mfumo mpya wa uhasibu na utoaji taarifa katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Hamid Njovu, aliyekuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mafunzo ya Mfumo mpya wa uhasibu na utoaji taarifa katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma kwa Halmashauri za Wilaya ya Sumbawanga, Kalambo, na Manispaa ya Sumbawanga.

"Nimefurahishwa na jitihada ya Serikali na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kuandaa mafunzo haya baada ya kuona changamoto za uwekaji kumbukumbu za fedha na utoaji taarifa kwenye vituo vya kutolea huduma katika Halmashauri zetu, hususani katika sekta ya elimu na afya," amesema Njovu.

Akiongea na washiriki wa mafunzo hayo, Njovu amewasisitiza waratibu wa elimu wa kata kwamba taifa linawategemea wao kwenda kufundisha, lengo likiwa fedha zinazoenda katika vituo vya kutolea huduma zinafanyiwa kazi husika na taarifa zake zinawekwa katika kumbukumbu nzuri na zirudi katika ngazi ya Halmashauri ili kujua nini kinachofanyika.

Ameongeza kuwa ni jambo la busara kwa USAID na TAMISEMI kuwaamini watendaji wa elimu kata na watumishi wa Afya katika vituo vya kutolea huduma kwamba wanao uwezo wa kuendesha mafunzo hayo katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma.

"Fedha zinatumwa, je kuna watu ambao watazisimamia? USAID wamekubali kutoa mafunzo wakiamini kwamba kila kituo cha kutolea huduma kina uwezo wa kutunza fedha hizo," ameongeza Njovu.

Aidha, Njovu amesema kuwa sheria ya fedha inazitaka Halmashauri kutoa taarifa, lakini nyingi zinakuwa zina mapungufu. Ameongeza kuwa kwenye mgogoro mkubwa ni pale ambapo ruzuku zinazotolewa haziendani na taarifa za mapato na matumizi.

"Watu hawa wametambua changamoto tulizo nazo na wanaamini kwamba tunaweza kutoka hatua moja hadi nyingine, hivyo kwa mafunzo haya inabidi kuonyesha kwamba tunaweza kutekeleza suala hili," amesisitiza Njovu.

Mkurugenzi Mtendaji huyo amesema amefurahishwa kwamba mfumo huu mpya utawajengea watumishi wa vituo vya afya nidhamu ya matumizi, na kueleza kuwa mtumishi akiwa na nidhamu huwezi kuwa na tamaa ya kutaka kujinufaisha katika fedha za ruzuku.

Ameongeza kuwa mafunzo haya yataimarisha uwajibikaji kwa watumishi kwa kiasi kikubwa, na kuchangia kutoa huduma bora kwa jamii, na zaidi ushirikishwaji wa wananchi katika mapato na matumizi.

Katika mahojiano na washiriki wa mafunzo hayo, mmoja wa washiriki ambaye ni mtendaji wa elimu kata ya Mazwi, Victoria Fumpa, ameeleza kwamba amejifunza sana kupitia mafunzo hayo na kuahidi kutekeleza jukumu hilo sawasawa na mafunzo ya siku mbili yaliyofanyika katika mkoa wake wa Rukwa.

***Imeandikwa na Jacqueline Sombe, PS3***




***Meneja Mradi wa PS3 kwa Mkoa wa Rukwa, Bi. Rose Mangilima, akitoa ufafanuzi kwa washiriki wa mafunzo ya FFARS wakati wa kipindi cha mafunzo hayo mjini Sumbawanga. (Picha: Jacqueline Sombe)***

*KUTOKA MBEYA:*

# FFARS Yaleta Suluhu ya Hesabu za Fedha Katika Vituo vya Kutolea Huduma

Jitihada ya kuandaa na kuendesha mafunzo ya mfumo wa uhasibu na utoaji wa taarifa kwenye vituo vya kutolea huduma (FFARS) imekuwa na faida lukuki kwa watendaji wa elimu kata ambao ni waangalizi wa shule kwa kila kata, na wahudumu wa afya katika vituo vinavyotoa huduma ya kiafya.

Hili limethibitika pale ambapo mafunzo ya hatua ya kwanza yalifanyika mkoani Mbeya ambayo yalihusisha Waratibu wa Elimu wa kata pamoja na Maafisa Afya kutoka katika vituo vya afya katika Halmashauri za Mkoa wa Mbeya.

Katika mahojiano na jarida hili, Mratibu wa Elimu Kata ya Ilembo iliyopo Mbeya Vijijini, Bi. Ntabuli Mwakifuna anaeleza kuwa yeye binafsi mafunzo haya yamemjengea ujasiri wa kuweza kufanya ufualitiaji na uwezo wa kuhoji mapato na matumizi katika shule zilizopo katika Kata ya Ilembo, ambapo anasema hapo awali alikuwa hana ufahamu mzuri kwa baadhi ya fomu ambazo zilikuwa ni ngumu kueleweka kujaza.

"Mafunzo haya yamenisadia sana kwani sasa nimeelewa vyema na kupata uwezo wa kujaza madaftari yote ya fedha, hundi na taarifa za kibenki, na imenijengea uwezo wa kufanya hata ukaguzi," amesema Bi. Mwakifuna.

Kwa upande wa ushirikishwaji wananchi, Bi. Mwakifuna amesema hapo mwanzo haukuwa thabiti kwani walishirikishwa wale waliomo katika kamati ya shule na si wananchi wote kwa ujumla, lakini mafunzo ya FFARS sasa yamewawezesha pia kufahamu umuhimu wa kuwashirikisha wananchi wote kwa ujumla kuhusu mapato na matumizi.

Bi. Mwakifuna ameeleza pia changamoto nyingi ambazo amekutana nazo, ikiwa ni pamoja na kuwepo na matumizi zaidi ya fedha kuliko fedha zinazokuja. Hili, anasema, linatokana na kutokuwa na mfumo mzuri wa kuainisha matumizi, hivyo inampelekea mwalimu mhusika, hasa mwalimu mkuu kutumia fedha zaidi bila kuwa na uhakika wa kurudishiwa fedha zake hizo.

Naye Vitalino Joseph Kayombo, Msimamizi Msaidizi wa Kituo cha Afya Ilembo, ameeleza kuwa hapo awali alikuwa anapata sana changamoto ya kuandika mpango wa fedha katika mfumo uliokuwepo, kwani ulikuwa ni mgumu. Baada ya kupata mafunzo ya FFARS, amepata matumaini makubwa.

"Tumepata changamoto kwa muda mrefu katika suala la usimamizi wa fedha; fedha zinakuja kituoni lakini changamoto inakuja katika kuzisimamia, hasa kwakuwa tuna uhaba wa mtaalam wa mahesabu. Lakini mfumo huu ulioboreshwa utatuwezesha hata tusio na hii taaluma kuifanya kazi hii vizuri," amesema Kayombo.

Katika sekta ya Afya na Elimu nchini Tanzania kumekuwa na mifumo mbalimbali ya utunzaji kumbukumbu na mahesabu ambayo imekuwa inatumika kwa muda mrefu, ingawa imekuwa na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikisababisha Halmashauri kuwa na taarifa zisizo nzuri katika kutunza hesabu za mapato na matumizi, hasa katika sekta ya Afya na Elimu.

Pamoja na kuwepo Mifumo ya awali, Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma, ukishirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) ukaona ni vyema kutengeneza mfumo mpya ambao umerahisishwa kwa matumizi, hata kwa mtu ambaye hana taaluma ya mahesabu.



***Wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Lolezi jijini Mbeya wakifurahia uwepo wa mafunzo ya uhasibu kwa watumishi wa shule yao, wakiamini yataimarisha usimamizi wa fedha za ruzuku zinazotoka Serikalini. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision)***

***Imeandikwa na Jacqueline Sombe, PS3***

***KUTOKA DODOMA:***

# FFARS Kuchochea Huduma Bora za Afya, Elimu Tanzania

Mpango wa Serikali wa kupeleka fedha moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma utaviwezesha vituo husika kuitoa huduma hiyo kwa ufanisi na katika viwango vinavyotakiwa.

Hayo yamesemwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Bi. Rehema Madenge, wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya siku mbili ya wakufunzi wa mfumo mpya wa Uhasibu na Utoaji Taarifa za fedha kwa ngazi ya kituo cha kutolea huduma, *'Facility Financial Accounting and Reporting System'* – FFARS.

"Mfumo huu wa uhasibu na utoaji taarifa kupitia mpango wa Serikali wa kupeleka fedha moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma utasaidia wananchi wenye uhitaji kupata huduma bora za afya na elimu, kwakuwa mfumo huu umelenga kuviwezesha vituo hivi kupanga na kuratibu matumizi yao ya fedha," amesema Bi Madenge.

Amesema kuwa mfumo umeanza na sekta hizo mbili kwakuwa hizo ndizo ambazo Serikali imeweka kipaumbele, ili ziweze kusaidia kutoa huduma zinazostahili na bora kabisa kwa wananchi.

Ameongeza kuwa mpango huo ni mahususi kwa ajili ya kuboresha huduma kwa wananchi kwasababu kupitia mfumo huo, vituo vitaweza kupanga matumizi yao kulingana na namna huduma hizo zinavyohitajika, pamoja na changamoto zilizopo.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mratibu wa Huduma za Afya Wilayani kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dkt. Sijenunu Aaron, amesema mfumo huo utawezesha vituo kupanga mipango yao wenyewe ya fedha tofauti na ilivyokuwa awali ambapo Halmashauri zilikuwa zinapanga kwa niaba yao.



***Mafunzo kwa watumishi wanaohusika na masuala ya fedha yakifanywa na Mratibu wa Elimu Kata katika zahanati iliyoko Wilayani Kasulu, mkoani Kigoma. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision)***

Ameongeza kuwa utaratibu huo utavisaidia vituo kuboresha zaidi huduma zao kwa wananchi kulingana na mipango na matumizi yao ya fedha.

Dkt. Aaron amesema mafunzo ya FFARS yatawajengea uwezo watoa huduma namna ya kuratibu matumizi ya fedha, lakini pia kuwa na taarifa za matumizi ya fedha, jambo alilodai litasaidia fedha kutumika kulingana na malengo na mipango iliyokusudiwa na hivyo kuwezesha wananchi kupata huduma bora.

Kwa upande wake, Mhasibu Mwandamizi Elimu kutoka Wilaya ya Kilosa ambaye ni mkufunzi mshiriki wa mafunzo hayo, Bi Albertina Bata, amesema mafunzo yatasaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili watendaji, hasa uandaaji wa taarifa za mapato na matumizi ya fedha zinazotumika katika vituo vya kutolea huduma.

"Serikali imeshaanza mpango wa elimu bila malipo na fedha zimekuwa zikija moja kwa moja katika shule za msingi na sekondari, lakini kumekuwa na changamoto kwa walimu katika kutoa taarifa za fedha hizi kutokana na kutokuwa na ujuzi wa namna ya kuziandaa," amesema.

Ameongeza kuwa mfumo huo utachochea upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi ambapo wao kama wakufunzi watawezа kuitoa elimu waliyoipata katika ngazi za chini.

***Imeandikwa na Gladys Mkuchu, PS3***

### *MAKALA MAALUMU YA UIMARISHWAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA*

# PS3 Yazidi Kung'ara katika Halmashauri Tanzania

Huu ni Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma, ujulikanao kama PS3 kutokana na Kiingereza chake kuwa *Public Sector Systems Strengthening*. Mradi unayo majukumu makuu kama inavyojipambanua katika makala hii.

Utekelezwaji wa PS3 umejikita katika maeneo matano, ambayo ni: Utawala Bora na Ushirikishwaji wa Raia, Rasilimali Watu, Rasilimali Fedha, Mifumo ya TEHAMA, pamoja na Tafiti Tendaji.

Katika eneo la Utawala Bora na Ushirikishwaji wa Raia, matarajio ni kuwa na utawala uliooimarishwa katika ngazi ya kitaifa na katika halmashauri, ili kuweza kutumia rasilimali kwa uwazi, kuwezesha ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kufuatilia, na kutoa matokeo katika kila sekta. Eneo hili linachagizwa na kuongezwa kwa uwazi wa taarifa za Serikali, hasa pale mradi wa PS3, kwa kushirikiana na Serikali kuamua kuzitengenezea halmashauri na mikoa kote nchini tovuti kwa ajili ya kutangaza shughuli za Serikali ili wananchi wajue Serikali yao inafanya nini.

Shabaha kuu ya eneo la Rasilimali Watu ni kuongezeka kwa usawa wa mgawanyo wa rasilimali watu kwa ajili ya utoaji huduma bora kwenye maeneo yenye uhitaji zaidi, lakini vilevile kuimarisha mfumo wa ajira pamoja na kudumisha watumishi katika ajira Serikalini.



***Baadhi ya watumishi wa Shule ya Sekondari ya Loleza jijini Mbeya, wakipata mafunzo ya FFARS kutoka kwa Mratibu wa Elimu Kata jijini humo. (Picha: John D. Lyimo wa True Vision)***

Kwenye Rasilimali Fedha, matarajio ni ongezeko la pato la ndani kwa ajili ya huduma za umma, na ongezeko la matumizi ya fedha kwa maana ya ufanisi, na thamani ya fedha katika kutoa huduma. Eneo hili likijizatiti, ndio eneo hasa litakalosaidia katika kuimarika kwa utoaji wa huduma za jamii kama vile afya, elimu, na miundombinu.

Hakuna Maendeleo yoyote bila watu kuwasiliana, hivyo basi PS3 wameweka pia nguvu zao katika Mifumo ya Mawasiliano, ikiwa na matarajio ya kuimarisha mifumo ya mawasiliano iliyopo nchini na matumizi ya takwimu na taarifa kwa wadau kufika kwa wakati.

Kuna eneo la Tafiti Tendaji. Hili ni eneo muhimu kufanyika kwa tafiti ambazo zitatumiwa kuzungumzia changamoto zilizopo, pamoja na kutoa taarifa za kusaidia kwenye maamuzi.

Katika hayo yote, majukumu ya utendaji kazi yapo kulingana na ngazi husika, mathalani kwenye ngazi ya Taifa ni kuendeleza majadiliano ya kisera na uimarishaji mifumo katika wizara, idara na taasisi mbalimbali za Serikali. Hii inajumuisha sekta ya afya, pamoja na sekta nyingine ambazo PS3 inafanya kazi.

Mradi wa PS3 ulio kwenye Mikoa 13 na Halmashauri 93 nchini, ukiwa na lengo la kuimarisha mifumo ya sekta za umma katika ngazi ya Halmashauri, ulianza Juni, 2015, na unafadhiliwa na watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID). Umekuwa faraja na mkombozi kwa Halmashauri na mikoa kote nchini, hususan hizi Halmashauri 93 na Mikoa 13 ambapo umejikita zaidi.

Matokeo ya Mradi wa PS3 yamekwishaanza kuonekana. Katika Halmashauri ya WIlaya za Magu na Buchosa, kwa mfano, wapo mashuhuda wa mafanikio ya Mradi huu wanaokiri manufaa ya mifumo kuimarishwa. Moja ya maeneo yaliyoimarishwa ni utengenezwaji wa tovuti kwa Halmashauri na Mikoa yote nchini.

"Tulipokea Mashuka 150, kutoka kwa mtu aliyetusoma katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

***Inaendelea ukurasa unaofuata***

*MAKALA MAALUMU YA UIMARISHWAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA*

# PS3 Yazidi Kung'ara katika Halmashauri Tanzania

***Inatoka ukurasa uliopita***

Hiyo imesaidia kuokoa fedha kiasi cha shilingi 1,500,000/- ambazo kwa sasa zitaelekezwa kwenye matumizi mengine, hususan masuala ya vifaa tiba," anazeleza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Lutengano Mwalwiba.



***Afisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, Mwalimu Abichi Chacha, akizungumza na mwandishi wa Makala hii wakati wa mahojiano. (Picha: Jacqueline Sombe, PS3)***

Lutengano anakiri kuwa mbali ya kupata mashuka 150 ambayo yatasaidia katika kutoa huduma kwa wananchi wa Magu, mapato nayo yamepanda kutokana na kuimarishwa kwa mifumo.

"Mathalani nikwambie tu kwamba kabla ya mifumo, mapato ya juu kabisa katika Halmashauri yalikuwa shilingi milioni 95 kwa mwezi, lakini sasa tunakusanya hadi shilingi milioni 215, haya ni mafanikio makubwa," anakiri Mwalwiba.

Anaongeza kuwa kwa upande wa Hospitali nako kiasi cha mapato kimeongezeka kutoka shilingi laki sita kwa wiki, hadi shilingi milioni 2.4.

Mkurugenzi huyo anasema ujio wa PS3 sio tu umewaamsha kutoka usingizini, bali zaidi sana umewaongezea morali, kwani hapo awali Halmashauri ilikuwa na mashine za kukusanyia mapato zipatazo mbili tu, lakini kwa hivi sasa imejizatiti hata kununua mashine 67 za kielektroniki za kukusanyia mapato (Point of Sales – POS), huku ikipanga kufikisha mashine zipatazo 100.

Wilaya ya Magu ambayo sasa inaimarishiwa mifumo kwa kufungiwa mtandao kiambo, ni mfano mwingine wa namna mifumo inavyoendelea kuimarishwa na PS3. Hilo litawezesha Halmashauri kuwa na sehemu 25 za utumiaji wa mtandao kutoka sehemu 10 zilizokuwepo hapo awali.

Mtaalamu wa mifumo katika Halmashauri hiyo, Surumbu Emmanuel, anakiri kuwepo kwa miundombinu ambayo ilikuwa chakavu.

"Kwakweli hatuna lugha nzuri ya kusema, lakini yatosha kuwashukuru sana PS3. Kabla ya mifumo kuanza kuboreshwa kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa kazi, mfano watu wa malipo na watu wa mapato walilazimika kutumia sehemu moja kutokana na uhaba wa miundombinu," anaeleza.

Surumbu anakiri kwamba zaidi ya shilingi milioni 15 ambazo zilitakiwa zibebwe kwenye bajeti ya Serikali katika kuimarisha mifumo ya Halmashauri, hususan suala zima la mtandao kiambo, zimebebwa na PS3, na sasa fedha hizo zitaelekezwa kwenye shughuli nyingine za maendeleo kwa manufaa ya wananchi wa Magu.

Kwa upande wake, Mwalimu Abichi Chacha ambaye ni Afisa Elimu Vielezo na Takwimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, kama walivyo watu wengine, anaona mwanga bora kwa ufadhili wa PS3.

"Ilitulazimu kufanya kazi usiku wa manane ili kupishana na watu wa ofisi zingine, kwakuwa nyakati za mchana kazi isingewezekana kutokana na mtandao kuwa chini uliosababishwa na watumiaji wengi. Kufungwa kwa LAN ni neema kubwa kwetu," anasimulia.

Mwl. Chacha anasema kwamba walikuwa wakichukua muda mrefu sana kufanya kazi ya kurekodi taarifa za shule kwenye mfumo wa BEMIS. Kwa kawaida kazi hiyo hupangwa kufanyika kwa siku mbili, lakini kwa Buchosa ilichukua takribani siku sita kukamilisha kazi hiyo kutokana na changamoto ya upatikanaji wa mtandao.

"Isingewezekana kufanya kazi hii mchana, maana mtandao ulikuwa chini sana. Kwa maeneo yenye mtandao madhubuti, kazi ya ku-'upload' kitu huchukua sekunde nane tu uwapo eneo kama Jiji la Mwanza au Ilemela na maeneo mengine ya mijini, lakini hapa Buchosa sisi tulitumia kati ya sekunde 100 hadi 120," anakumbuka.

Edward Mwasakafyuka ni Afisa TEHAMA wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa. Anakumbuka jambo moja lililokuwa likimsumbua sana kichwa: "Kuna wakati zinakuja kazi za presha, inatulazimu kuhamisha ofisi kutoka hapa Buchosa kwenda Sengerema au hata wakati mwingine kwa Katibu Tawala."

Kwa sasa, mifumo iliyoimarishwa imeleta faraja kwa wafanyakazi wa Halmashauri hizo.

***Imeandikwa na Atley Kuni wa TAMISEMI***

# MIFUMO YETU